## NJIA ZA MAWASILIANO:

- Zipo njia mbalimbali za kuanzisha/kuchochea mawasiliano na watoto au kujibu kile watoto wanachotaka kuwasiliana nasi tangu wakiwa wachanga. Kwa mfano:
  - *kuongea*
  - *kugusa*
  - *kuimba*
  - *kutazama (machoni)*
  - *kutumia ishara mbalimbali usoni*
  - *ishara/ vitendo mbalimbali*
  - *kubadili sehemu/mazingira ya mtoto*
  - *kutembea*
  - *mirindimo ya sauti na midundo kama vile kuimba,kupiga makofi*
  - *kutabasamu*
  - *kucheza*
  - *kumuiga mtoto nk.*
- Mara zote inashauriwa kutumia njia ambayo inafaa kutegemeana na uwezo wa mtoto au hali aliyonayo mtoto kwa wakati huo.
- Mfano: Kutumia sauti ya utulivu pale mtoto anapotaka kulala au pale anapolia, AU kutumia sauti ya juu au kupiga makofi/kuonyesha hali ya uchangamfu pale mtoto anapokuwa katika hali ya furaha au anapenda kucheza.

## MAHITAJI YA KUWASILIANA:

- Mara zote ujibu kile afanyacho mtoto katika kuwasiliana nawe kwa makini sana na huruma (Mfano, kwa kuongea, kumgusa, kutumia ishara mbalimbali usoni, kutumia ishara/vitendo mbalimbali vya kimawasiliano).
- Chochea mawasiliano na mtoto (Mfano kumuongelesha, kumgusa gusa, kumtazama machoni, kumwimbia nk).




## KUWASILIANA KWA NJIA/MILANGO YA UFAHAMU:

- Unaweza kuwasiliana na mtoto kwa kutumia njia/milango mbalimbali ya ufahamu au kuchochea ukuaji wa njia/milango ya ufahamu kwa watoto.
- Kuchochea kuona kwa mtoto kwa njia ya kutazamana na mtoto machoni, kutabasamu, kuchezesha ulimi, n.k
- Kuchochea hisia mbalimbali za mwili kwa kumkuna kuna kwa uangalifu au kumgusa, au kumfanyia masaji, nk.
- Kuchochea ukuaji na ufanyaji kazi viungo mbalimbali vya mwili kwa kumrusha rusha, kumchezesha chezesha mikononi kama vile anabembea.
- Kunusa.



## HALI AU TABIA ZISIZO ZA KAWAIDA:

- Kuzungusha kichwa.
- Kukaa kimya kwa muda mrefu.
- Kujitenga na wenzake.
- Uwe makini na tabia zisizo za kawaida kwa watoto. Unapoona mtoto anaonyesha tabia zisizo za kawaida ni vizuri kumtazama kwa makini sana.
- Usidharau tabia zisizo za kawaida kwa sababu zinaweza kuwa ishara ya kuchelewa kukua kwa mtoto.



## KUKUA KWA LUGHA:

- Anzisha/chochea mawasiliano na mtoto kadri anavyoweza.
- Watoto wanaweza kuchelewa kuzungumza na kwamba kila mtoto ana wepesi wake katika kujifunza lugha.
- Endapo unapenda kumsaidia mtoto kuzungumza mwonyeshe mawasiliano yenye hisia chanya katika kutengeneza maana za maneno.
- Mara zote msaidie mtoto katika jitihada zake za kuwasiliana na muonyeshe kuwa unajali kile anachojaribu kuwasiliana nawe hata kama si sahihi.
- Mfano: Matamshi kama 'mma' tamka 'mama' 'maji'.

## MIEZI 0-3:

- Uwe msikivu/mfuatiliaji wa karibu sana wa ishara mbalimbali za kimawasiliano anazozionyesha mtoto.
- Mfano: Kulia kwa ukali kusiko kwa kawaida kwa mchanga.

## MIEZI 4-6:

- Cheza na mtoto michezo yenye kuhusisha mtu na mtu, yenye midundo ya kimuziki (mfano, kupiga makofi) na nyimbo ambazo zinajenga mahusiano na kukua kwa lugha.
- Kuwa muangalifu na hali/hisia za mtoto pale unapochagua namna ya kucheza au wimbo.

## MIEZI 6-9:

- Msaidie mtoto kutafuta vitu mbalimbali katika mazingira (mfano kumuonyesha vitu au kufikia vitu) kwa hisia chanya.
- Msaidie mtoto pale anapojaribu kusogea lakini umwache ajaribu kutatua changamoto anazokutana nazo mwenyewe (mfano, kugeukia tumbo).
- Mpatie michezo yenye kuhusisha mtu na mtu yenye midundo ya kimuziki na kuhusisha mwili mzima.

## MIEZI 9-13:

- Msaidie mtoto katika kutafuta/kuona vitu mbalimbali katika mazingira yaliyo nje na aliyoyazoea.
- Mwonyeshe mtoto kile unachofanya pale unapomuona anapendelea kuona kile ufanyacho (mfano kuwaonyesha namna ya kutumia vitu hivyo).

## MIEZI 13-24:

- Wapatie watoto mazingira ya kuwawezesha kushirikiana (mfano waache washiriki kwenye kazi mbalimbali ufanyazo).
- Wapatie watoto mazingira ambayo kwayo wanaweza kujifunza juu ya mazingira. Mfano, kuonyesha na kutaja vitu mbalimbali.





## MAELEZO KWA AJILI YA MAWASILIANO

**KWA MAELEZO ZAIDI WASILIANA NA:**

**KITUO CHA WATOTO YATIMA IRENTE**
**SIMU:**

**0754 844 777**
**0714 157 837**

**MHUSIKA:**

________________________________

________________________________

Sebastian Kolowa Memorial University SEKOMU — IRENTE CHILDREN'S HOME — Leibniz Universität Hannover

© 2019 Prof. Dr. Ulrike Lüdtke,
Leibniz Universität Hannover
– All Rights Reserved –

ulrike.luedtke@ifs.uni-hannover.de

Niedersächsisches Ministerium für Soziales, Gesundheit und Gleichstellung

Kipeperushi hiki kimetengenezwa kwa msaada wa Wizara ya Ustawi wa Jamii, Afya na Fursa Sawa ya Jimbo la Lower Saxony, Ujerumani

**MAFUNZO YA MALEZI YA AWALI NA MAKUZI YA MATAMSHI NA LUGHA
KITUO CHA WATOTO YATIMA IRENTE,
FEB 2018 - SEP 2019**




# UKUAJI WA LUGHA WA MTOTO

Tunawashukuru washiriki wote wa Mafunzo kwa kutunga maudhui na kupigapicha mbalimbali zilizomo kwenye kipeperushi hiki.

Kwa sababu za kimaadili, tunadiriki kutoonyesha sura za watoto walioko kwenye picha.